TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo, Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam

“Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote”

Kumb na: Taro /P/2022/ A18 **: Swahili Version:** Tarehe: 13 Agosti 2022

# “KUMTAKA MSANII TUNDAMAN KUOMBA RADHI KWA TUHUMA ZA SIMBA DAY (UWANJA WA TAIFA) NI KUMINYA UHURU WA KUJIELEZA KWENYE KAZI ZA SANAA

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **“TAASISI YA HAKI ZA WASANII”** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa kushughulikia haki na maslahi ya wasanii wote Tanzania.

Mnamo tarehe 08/08/2022 Msanii wa muziki wa kizazi kipya **(Khalid Ramadhani)**, maarufu kama **TUNDAMAN**, alitumbuiza uwanja wa taifa **(Simba Day).** Katika utumbuizaji wake alihusisha sanaa ya maigizo kabla ya kuanza kuimba. Ambapo maigizo hayo yalibeba maudhui yanayofanana na utaratibu wa misiba kwa watu wenye imani ya Kikristo. **Tundaman** Aliingia uwanjani akiwa amebebwa ndani ya jeneza, likitanguliwa na msalaba uliobebwa na muigizaji aliyefungwa kamba mwenye asili ya ualbino. Jeneza lilifikishwa jukwaani, Msanii aliyeigiza kama mchungaji alitoa wasifu wa marehemu, kisha akaruhusu jeneza lifunguliwe kwa ajili ya marehemu kuagwa, lilipofunguliwa, Msanii **Tundaman** alianza kuimba akiwa ndani ya jeneza na kustaajabisha halaiki ya watazamaji waliokuwepo uwanjani.

Mnamo tarehe 10/08/2022, Uongozi wa timu kongwe ya mpira wa miguu nchini (**Simba Sports Club)** walitoa taarifa kwa umma, kupitia mtandao wao wa kijamii (instagram), kuwataka wasanii wote walioshiriki kwenye utumbuizaji wa **Tundanman** siku ya Simba Day kuomba radhi, kwa wanachokidai kuwa ni kosa.

Mnamo tarehe 11/08/2022, **Chama cha Watu wenye Ulemavu Tanzania (TAS)** kwa pamoja na **Kituo cha Haki za Binadamu (Legal and Human Rights Centre-LHRC)** kupitia mitandao yao ya kijamii (instagram), walitoa tamko la kulaani vikali kitendo kilichofanywa siku ya Simba Day cha kutumia jeneza, msalaba na kumtumia mtu mwenye ualbino na kumfunga mikono kama msukule. Ambapo waliwataka **Simba Sports Club** kuomba radhi kwa kitendo cha kinyama, kikatili na kibaguzi.

## HOJA ZA KISHERIA

A. **Je kitendo cha Tundaman na wasanii wenzie kutumia jeneza na msalaba katika maigizo ni kosa ?**
Ifahamike ili kitendo kiwe kosa la jinai, lazima kiambatane na mambo makuu mawili ambayo ni (i) Nia ovu ya kufanya kitendo kinachokatazwa na sheria **(mens rea**) (ii). Kufanyika kwa kitendo kinachokatazwa na sheria **(actus reus).** Vipengele vyote viwili

vinapaswa kuthibitishwa pasipo shaka ili kuwepo kwa kosa la jinai. Kwa mujibu wa mahojiano aliyofanyiwa Tundaman na chombo cha habari **(JembeSport)**, yaliyowekwa **YOUTUBE** 12/08/2022**,** Saa 10:54. Nukuu maneno ya Tundaman ***"Wakati nafanya sikutegemea kwamba nitamuudhi mkristo"***. Hii inasanifu kuwa Tundaman hakuwa na **Nia ovu** ya kufanya kitendo kinachokatazwa na sheria.

i. Kwa mujibu wa kifungu cha **125** cha **Sheria Ya Makosa Ya Jinai**, **Sura ya 16, Mapitio ya mwaka 2019**, kinaelezea kuhusu **kutukana dini**. Kinaeleza kuwa ***mtu yoyote atakayeharibu, kujeruhi au kunajisi sehemu yoyote ya ibada au kitu chochote kinachochukuliwa kitakatifu na tabaka fulani la watu, kama mtu huyo atafanya hivyo kwa lengo la kutukana dini au tabaka fulani la watu au kama atafanya hivyo akifahamu kuwa kuharibifu, kujeruhi na kunajisi huko kutachukuliwa na tabaka fulani la watu kuwa ni kutukana imani yao, Basi mtu huyo atatiwa hatiani kwa kosa la jinai***.

   Vifungu vingine vya sheria hiyo tajwa yaani kifungu cha **126, 127, 128** na **129** vinaongelea (i) vurugu kwenye mkusanyiko wa kidini (ii) kuingilia mazishi au sehemu za imani ya kidini kwa lengo la kutusi imani ya kidini au kuumiza hisia za watu, (iii) kuzuia mazishi na (iv) kuzungumza maneno kwa nia ya kuumiza hisia za watu wenye imani fulani ya kidini.

ii. Kwa mujibu wa kifungu cha **2** cha **Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230,** kinachoelezea maana ya neno **"michezo ya kuigiza",** kikisomeka pamoja na kanuni ya **16 (1)(o)** ya **Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza Mwaka 2020.** Kanuni hiyo ya **16 (1)(o)** inaelekeza kuwa bodi ya filamu haitotoa kibali cha kutayarisha, kusambaza au kuonesha filamu, mchezo wa kuigiza au tangazo lolote la filamu au mchezo huo endapo maudhui yatahusisha *"kutukuza au kuhalalisha ubaguzi wa rangi, ukabila, udini, jinsia, elimu, ulemavu, kiuchumi au ubaguzi mwingine wa aina yoyote*"

**B. Je mtu mwenye asili ya ualbino kuigiza kuwa amefungwa mikono kama msukule ni kitendo cha kinyama, kikatili na kibaguzi?**

i. *Kabla ya kujadili hoja hii tujiulize, je mtu asiyekuwa na asili ya ualbino, angeigiza kufungwa mikono kama msukule ingekuwa kitendo cha kinyama, kikatili na kibaguzi?"*. Ifahamike kuwa kuigiza ni kazi kama kazi nyingine halali kisheria. Msanii mwenye asili ya ualbino anayo haki ya kufanya kazi za sanaa ya kuigiza kama watu wengine bila kutafsiriwa tofauti.

ii. Kwa mujibu wa ibara ya **12(1)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(1977)** kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, inaelekeza *kuwa "Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa"*. Ibara ya **13(1)** ya katiba tajwa inaelekeza kuwa "*watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ubaguzi wowote, kulindwa, kupata haki sawa mbele ya sheria.* Ibara ya **22(1)** ya katiba tajwa inaelekeza kuwa *"kila mtu anayo haki ya kufanya kazi*

**C. Je kuwalazimisha Tundaman na wasanii wenzie waliotumbuiza Simba Day kuomba radhi ni sawa kisheria?**

i. Kwa mujibu wa ibara ya **13(6)(a)** ya **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(1977)** kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, inaelekeza kuwa *"Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya **kusikilizwa kwa ukamilifu,** na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya sheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika*

ii. Kwa mujibu wa kanuni ya **30(1)** ya **Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza Mwaka 2020,** inaelekeza kuwa mtu yoyote, chama, shirikisho, au asasi yenye ushahidi kuwa mchezo wa kuigiza kwenye tamasha umesababisha madhara kwenye jamii, awasilishe malalamiko rasmi kwa maandishi katika Bodi ya filamu.

**<u>HITIMISHO:</u>**

Kitendo cha Tundaman kuingia na msalaba na geneza uwanjani siku ya Simba Day, Hakikidhi viwango vya kutengeneza kosa la jinai la **kutukana dini** wala **makosa mengine ya namna hiyo** kama yalivyoorodheshwa na sheria ya Makosa ya Jinai. Tundaman na wasanii wenzake hawakuaribu, hawakujeruhi wala hawakunajisi MSALABA. Hawakuongea neno wala kufanya kitendo chochote kilichoelekezwa kushambulia imani ya dini ya wakristo au kuumiza hisia zao. Hivyo basi hawakutenda kosa lolote kisheria.

Kuwalazimisha wasanii hao kuomba radhi ni **ukiukaji wa haki za binadamu** (haki ya kujitetea) na **utawala wa sheria.** Sheria imeweka utaratibu wa kufuata endapo mtu ataamini ameumizwa na maigizo katika tamasha. Pia ieleweke kuwa, Muigizaji mwenye asili ya ualbino anayo haki ya kufanya kazi za sanaa ya uigizaji kama watu wengine. Akiigiza jambo lolote, inapaswa atafsiriwe kama waigizaji wengine wasio albino. Kitendo cha Kutafsiri maigizo yale kuwa ubaguzi ni kuwanyima haki wasanii wenye ualbino kushiriki kikamilifu katika shughuli za sanaa.

Vitendo vya baadhi ya watu katika jamii, kuwashambulia na kuwahukumu wasanii wa muziki kila wanapofanya ubunifu unaohusisha imani za kidini bila hata kuzikosea imani hizo, ni jitihada mahususi za kuminya na kudhoofisha wasanii katika kufurahia haki yao ya binadamu ya **UHURU WA KUJIELEZA KWENYE KAZI ZA SANAA (Artistic Freedom of Expression).** Pia ni uvunjifu wa haki za binadamu unaopaswa kupigwa vita na jamii. Uhuru wa kujieleza ni haki ya msingi ya binadamu inayolindwa na katiba ya nchi. **TARO** tunatoa rai kwa jamii kutokubali utamaduni wa kutumia imani za kidini kama ukuta wa kuzuia wasanii wa muziki kufurahia haki yao ya binadamu ya **uhuru wa kujieleza katika kazi za sanaa**. Jamii ikiruhusu mwenendo huu, tutawezesha maovu katika jamii kusitirika kwa mgongo wa imani za kidini, na hakuna msanii atakayethubutu kuyafichua katika kazi za sanaa.

**ASANTENI**
(Kazi iendelee)
Wako katika kujenga Taifa

Mkurugenzi Mkuu wa Utawala
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**